**Arafa ya sera**

Nambari 32 Juni 2013

Taasisi zilizoshirikiana: Wizara ya Afya ya Umma na Usafi na Taasisi ya Kumbukumbu za Idadi ya Watu (PRB)

# Kukomesha Ukeketaji wa Wanawake: Sheria ni Hatua tu ya Kwanza

Mwanamke mmoja kati ya wanne nchini Kenya amefanyiwa ukeketaji, licha ya Serikali kupitisha Mswaada wa Kuzuia Ukeketaji mnamo mwaka wa 2011, wasichana wengi bado wamo hatarini. Je ni nini zaidi kinachostahili kufanywa kukomesha tamaduni hii yenye madhara?

Ukeketaji wa Wanawake ambao unahusu kuondoa baadhi au sehemu yote ya uzazi (angalia kisanduku), inatambulika Kimataifa na kitaifa kama ukiukaji wa haki za wasichana na wanawake. Serikali ya Kenya imechukua hatua ya kupiga marufuku desturi hii- kwanza mnamo mwaka wa 2001 ilipoanzisha Sheria ya Watoto ambayo ilizipa mahakama uwezo wa kuadhibu wale wanaoshirikisha au kuendesha desturi ya ukeketaji na mnamo mwaka wa 2011, ilipopitisha Mswaada wa Kuzuia Ukeketaji. Kwa mujibu wa Takwimu za Utafiti wa Hali ya Watu na Afya nchini (KDHS), kuenea kwa desturi hii kulipungua kutoka aslimia 38 ya wanawake mnamo mwaka wa 1988 hadi aslimia 27 mwaka wa 2009.

Licha ya ufanisi huu, katika jamii ya Wasomali na ya Wakisii, zaidi ya aslimia 96 ya wanawake wa umri wa miaka 15 hadi miaka 49 wamefanyiwa ukeketaji na katika jamii ya Wamaasai karibu aslimia 73 ya wanawake wamefanyiwa ukeketaji.

Kulingana na ngariba mmoja wa ukeketaji kutoka jamii ya Wamaasai , *"Ukeketwaji wa wasichana ni jambo ambalo watu wetu wamelifanya kwa miaka mingi. Hakuna anayeweza kutushawishi eti ni makosa."*[1]

Arafa hii ya sera inamulika jinsi desturi hii inavyoendelea kufanyika katika maongozi na mpango wa mazingira ya wakati huu na inatafuta kujibu swali: Je ni nini zaidi kinachohitajika kufanywa ili kupunguza na hatimaye kukomesha desturi hii?

*Shirika la Afya Duniani linafafanua ukeketaji ambao wakati mwingine unajulikana kama kukata sehemu ya nyeti ya wanawake au tohara ya wanawake- kama kuondoa baadhi au sehemu yote ya uke ya nje au kujeruhi viungo vya uke wa wanawake kwa ajili ya mila au sababu yoyote isiyokuwa ya kimatibabu.*[2] *Aina tatu za ukeketaji zinafanywa nchini Kenya. Aina ya kwanza ni kuondolewa kwa kisimi, aina ya pili ni kuondolewa kwa kisimi na sehemu ya ndani ya uke na Aina ya tatu ni kuondolewa kwa kisimi, sehemu ya ndani na ya nje ya uke na ngozi kushonwa na kuacha tu tundu dogo.*[3] *Ukeketaji wanawake umeendelea sana miongoni mwa jamii kadhaa nchini Kenya na idadi hii ni kubwa hasa miongoni mwa jamii za Wasomali na Wakisii. Ni desturi yenye uchungu ambayo huleta madhara ya kiafya na matatizo ya kijamii kwa maisha ya wasichana, kama vile kuvuja damu kwa wingi, maambukizi na kiwewe cha hisia na kimwili.*

## Ukeketaji: Utamaduni dhidi ya Afya

Jamii zinazoendeleza ukeketaji nchini huihalalisha desturi hii kama njia ya kuingia utu uzima. Kwa mujimu wa ripoti ya Utafiti wa Hali ya Watu na Afya nchini (KDHS)2008-09 , jamii zinazoendesha desturi hii zinaamini kwamba tamaduni hii ni kitambulisho cha utamaduni wao, kuimarisha usafi,kuhimiza ubikira na heshima; huongeza nafasi ya wasichana kuolewa, hupunguza hamu ya ngono na ni mojawapo ya desturi za kidini.[4]

Kwa upande mwingine utafiti umebainisha kwamba ukeketaji unaathiri afya ya mwanamke kimwili na kimawazo.[5,6,7]

Wanawake wanaopitia hali hii hupata maumivu makali. Baadhi ya matatizo ya kiafya yanayotokana na ukeketaji ni pamoja na kutokwa na damu kwa wingi, maambukizi ya pepopunda, maradhi katika mfumo wa kutoa mkojo, kutozuia mkojo,vidonda, matatizo wakati wa kujifungua, na uchungu wakati wa ngono. Baadhi ya utafiti umeonyesha kwamba ukeketaji unahusika na uharibifu wa kibofu cha mkojo na kutokwa na damu kwa wingi wakati wa kujifungua. Maambukizi na matatizo wakati wa kujifungua kutokana na ukeketwaji kunaweza kusababisha kifo.

## Sera kuhusu Ukeketaji nchini Kenya

Serikali ya Kenya imeratibu maongozi kadhaa ya kukomesha ukeketaji. Mnamo mwaka wa 1983, Rais alitoa agizo dhidi ya ukeketaji. Wale waliokuwa wakiendesha desturi hii walihitajika kukoma au sivyo kuchukuliwa hatua za kisheria. Kutokana na hatua hiyo jamii nyingi ziliendelea na desturi hii kwa siri kwa kuwaalika wapashaji tohara kwa nyumba zao bila ya ufahamu wa serikali. Kwa hivyo, hata ingawa agizo hilo lilidhihirisha nia kuu ya kisiasa katika kukomesha ukeketaji nchini, halikuwa na ufanisi mkubwa.

Kufuatia azimio la Umoja wa Mataifa la mwaka wa 1993 kuhusu kukomeshwa kwa dhuluma za kila aina dhidi ya wanawake, Kenya ilibuni Mpango Makhususi wa kukomesha ukeketaji. Azimio hilo la Umoja wa Mataifa lilizihitaji Serikali kujitolea kushutumu dhuluma dhidi ya wanawake, kuadhibu wakosaji na kushughulikia maswala ya dhuluma za kijinsia.[8] Hatua hii ilileta msisimuko nchini Kenya katika kushughulikia ukeketaji, hatua ambayo ilitiliwa mkazo zaidi na Mkutano wa Kimataifa kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo (ICPD) jijini Cairo mnamo mwaka wa 1994 na Mkutano wa Nne wa Ulimwengu kuhusu Wanawake huko Beijing mwaka wa 1995. Kufuatia Mkutano wa Kimataifa wa Cairo, Kenya ilibuni maongozi ya idadi ya watu ambayo yalitambulika kama taarifa rasmi ya maongozi ya serikali nambari 1 ya mwaka 2000 kuhusu idadi ya watu na maendeleo endelevu ambayo yalipinga ukeketaji.[9]

Mnamo mwaka wa 2001, Serikali ilitunga sheria mpya ambazo zililenga kukabiliana na ukeketaji. Sheria ya watoto ambayo ilianza kutekelezwa mnamo mwaka wa 2001 ilizipa mahakama uwezo wa kuadhibu wale wanaoshirikisha au kufanya ukeketaji. Huku ukeketaji ukiendelea kupungua nchini Kenya, mmoja kati ya wanawake wane bado wanaendelea kufanyiwa ukeketaji. Hatua hii imeifanya Serikali kuanzisha sheria muafaka zaidi, kifungu cha sheria ya mwaka wa 2011 ya kuzuia Ukeketaji wa wanawake, ambayo inatoa amri ya kuwaadhibu vikali wanaokiuka sheria hii. Adhabu hii inajumuisha kifungo cha kati ya miaka mitatu hadi saba au faini ya takribani dola 6,000 kwa yeyote atakayepatikana akiendesha ukeketaji.[10] Mtu anayesababisha kifo kwa kufanya ukeketaji anastahili kifungo cha maisha. Mbali na hayo Maongozi ya Kitaifa ya Kukomesha Ukeketaji yalizinduliwa mnamo mwaka wa 2010. Maongozi hayo yanawahitaji washikadau kuchukua hatua muafaka kuimarisha hatua za kukomesha ukeketaji kupitia sheria, elimu kwa umma, kutetea, kutangazwa katika vyombo vya habari, kuwapa shime wanawake na kupatikana kwa huduma za afya ya uzazi na huduma nyingine zinazohitajika. Sheria hizi na maongozi yanaungwa mkono na katiba ya Kenya iliyozinduliwa mwaka wa 2010, ambayo inakariri kujitolea kwa Serikali kulinda na kuimarisha haki za kibindamu na uhuru wa kimsingi.[11] Kati ya nchi 27 zinazostawi ambako takwimu kuhusu ukeketaji zimetolewa, Kenya ni miongoni mwa nchi 17 ambazo zina sheria muafaka dhidi ya ukeketaji.[12]

## Ni miradi gani iliyopo ya kukomesha ukeketaji?

Tangu mwaka wa 1983 wakati agizo la kwanza la rais dhidi ya ukeketaji lilipotolewa, mashirika mbalimbali yasiyo ya serikali pamoja na yale ya kijamii yalianza kubuni mikakati ya kukomesha itikadi hiyo. Miongoni mwa shughuli za mashirika hayo zilikuwa kufanya utafiti, kutoa mafunzo kwa jamii na kuweka vituo vya kuwahifadhi wasichana. Mojawapo ya mbinu muhimu iliyozinduliwa katika miaka ya 1990 na chama cha mpango wa uzazi hapa nchini (FPAK) ilikuwa ni kutoa mbinu mbadala ya kuwawezesha wasichana kuingia katika utu uzima. Mbinu hii inatoa mafunzo kwa wasichana kuhusu maumbile yao, changamoto watakazokumbana nazo wanapovunja ungo, mahusiano na uwajibikaji kuhusu masuala ya ngono.

Lengo la mbinu hii ni kudhihirishia jamii kwamba wasichana wanaweza kubadilika kutoka maisha ya utotoni na kuwa watu wazima bila kukeketwa. Mwishoni mwa mafunzo hayo, sherehe hufanywa ambapo wasichana hao hutuzwa. Mashirika mengi yanatumia mbinu hii. Miradi inayojumuisha mbinu mbadala za kuingia utu uzima kwa wasichana pia inaweza kutumiwa kuwaelimisha ngariba kuhusu haja ya kukomesha tamaduni hii na kuwapa mbinu mbadala za kujikimu kimaisha.

Mbinu nyingine inayoweza kutumiwa kukomesha ukeketaji wasichana ni kufungua vituo ambapo wasichana wanaokwepa utamaduni huu wanaweza kupata hifadhi. Vituo hivi huwasaidia wasichana hao kuendelea na elimu yao au kupata mafunzo anuai huku vikishirikiana na jamii kutoa hamasisho kuhusu hatari za ukeketaji na

kuwahimiza wazazi kuwakubali wasichana hao wanaporejea nyumbani bila kuwalazimisha kukeketwa. Wasichana wengi wanaopata hifadhi kwenye vituo hivyo wamefaulu kukwepa ukeketaji na ndoa za mapema. Baadhi yao wamekuwa mfano bora wa kuigwa na jamii huku wakiwa wanaharakati dhidi ya ukeketaji.

Licha ya ukweli kwamba visa vya ukeketaji vinaendelea kupungua hapa nchini desturi sugu na kitamaduni miongoni mwa jamii zinazuia kukomeshwa kwa tabia ya ukeketaji. Na hata ingawa jamii zimepata habari kuhusu athari za ukeketaji, baadhi yazo bado zinaendelea na tamaduni hiyo. Hivyo basi baadhi ya wanaharakati wanaopinga ukeketaji wanapendekeza kwamba viongozi wa jamii na dini wanapaswa kushirikishwa katika juhudi za kukomesha utamaduni huo.

## Tofauti katika visa vya ukeketaji

Nchini Kenya karibu wanawake wote wanafahamu swala la ukeketaji huku asilimia 27 wakiwa wamefanyiwa tambiko hilo lililo na machungu mengi. Hata hivyo utamaduni huu hutofautiana pakubwa katika jamii mbalimbali. Ukeketaji hauruhusiwi kabisa katika baadhi ya jamii za humu nchini lakini unatekelezwa katika jamii nyingine.

Mchoro1 unaonyesha kwamba karibu wanawake wote kutoka jamii ya wasomali (98%) wamepashwa tohara. Kwa mujibu wa ripoti ya KDHS idadi ya wanawake waliokeketwa katika jamii hii iliongezeka kwa kiasi kidogo baina ya miaka 2003-2009.

**Mchoro 1:** Asilimia ya wanawake walio na umri wa miaaka 15-49 ambao wamepashwa tohara kwa jamii




Kutoka: Taasisi ya Kitaifa ya Takwimu Nchini Kenya na ICF International, Utafiti wa Hali ya watu na Afya nchini Kenya 2008-9. (KDHS)

Katika jamii ya waKisii zaidi ya asilimia 96 ya wanawake wamepashwa tohara. Kwenye baadhi ya jamii nyingine zinazoendelea na utamaduni huu, idadi ya visa hivyo imepungua katika muda wa miaka 10 iliyopita. La muhimu ni kwamba ukeketaji ulipungua kwa kiasi kikubwa sana katika jamii ya wamasaai kutoka asilimia 93 hadi asilimia 73 mnamo mwaka 2009.[13]

Utafiti wa KDHS umeonyesha kwamba miongoni mwa marika yote isipokuwa wale walio na umri wa kati ya miaka 45-49, ukeketaji umepungua katika kipindi cha miaka kumi kutoka 1998 hadi 2008. Kwa mujibu wa mchoro2, visa vya ukeketaji ni vingi zaidi (asilimia 49) miongoni mwa wanawake wa umri wa kati ya miaka 45-49 huku vikiwa

**Mchoro 2:** Asilimia ya wanawake ambao wamepashwa tohara kwa umri




Kutoka: Taasisi ya Kitaifa ya Takwimu Nchini Kenya na ICF International, Utafiti wa Hali ya watu na Afya nchini Kenya 2008-9. (KDHS)

vichache zaidi (asilimia 15) miongoni mwa wanawake wa umri wa kati ya miaka 15-19. Hata hivyo thuluthi moja ya wanawake waliokeketwa wanasema walipashwa tohara walipokuwa na umri wa kati ya miaka 14-18 na pia sio jamii zote zilizokuwa radhi kukomesha upashaji tohara wanawake.

## Mapendekezo

Bado kuna mengi yanayopaswa kufanywa ili kupunguza au kukomesha ukeketaji. Ili kuimarisha mbinu zilizoko na kubuni mbinu mpya ambazo zitakuwa na athari kubwa zaidi, baraza la kitaifa kuhusu idadi ya watu na maendeleo (NCPD) linapendekeza yafuatayo:

NCPD ni shirika la Serikali linalobuni na kuimarisha sera za idadi ya watu na kushirikisha shughuli zinahusiana kwa ustawi wa maendeleo nchini Kenya.

**NCPD**

**Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo**

S.L.P. 48994 - GPO, Nairobi 00100, Kenya

Simu: 254-20-271-1600/01

Kipepesi 254-20-271-6508

Baruapepe:info@ncpd-ke.org

**www.ncpd-ke.org**

Jarida hili limechapishwa kwa Ushirikiano wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya kimataifa (USAID) chini ya Mradi wa IDEA (No. AID-0AA-A-10-00009). Yaliyomo kwenye jarida hili yamekusanywa na Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD) na hayaangazii maoni ya Shirika la USAID wala Serikali ya Marekani.

- Katika muda wa miaka miwili ijayo wizara ya maswala ya jinsia ikishirikiana na wizara ya afya itazindua mfumo wa mashauriano kutathmini uwezo na udhaifu wa mbinu zinazotumiwa kupunguza visa vya ukeketaji. Shughuli hii itahusisha uchunguzi kubainisha ni kwa nini baadhi ya jamii zimerekodi kupungua kwa kiasi kikubwa visa vya ukeketaji na kukadiria endapo kuna mafunzo yanayoweza kupatikana kutokana na uzoefu wao. Mfano mzuri ni jamii ya wamaasai ambapo ukeketaji ulikwa umekithiri lakini utafiti wa KDHS umebainisha kwamba visa hivyo vilipungua kwa kiasi kikubwa.
- Katika muda wa mwaka mmoja ujao wizara za maswala ya jinsia pamoja na ile ya afya zinapaswa kuimarisha uhamasisho miongoni mwa jamii kuhusu madhara ya kiafya yanayotokana na upashaji tohara wanawake. Elimu hii ya umma inapasa kulenga watoto, wanawake na wanaume katika jamii ambazo bado zinaendeleza utamaduni huu. Ikiwa utoaji hamasisho miongoni mwa jamii utaimarishwa, kuna uwezekano kwamba visa vya ukeketaji vitapungua kwa kasi. Ili kuhakikisha mbinu hii inafaulu, viongozi wa kijamii na wakazi wanaopinga utamaduni huu wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuipigia debe. Hatua hii itaendelea hadi pale ukeketaji utakapokomeshwa.

## Hitimisho

Ili kuimarisha haki za wanawake na afya yao kote ulimwenguni, ukeketaji lazima ukomeshwe. Serikali ya Kenya imeeleza kujitolea kwake kuhakikisha utamaduni huu umekomeshwa kwa kuweka sera na miradi mbalimbali inayonuia kuafikia hayo lakini kufikia sasa ni mafanikio machache tu yaliyoafikiwa. Ili Kenya iweze kushuhudia mafanikio ya lengo hili katika miaka ijayo, lazima serikali, washirika wake wa kimaendeleo, mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya kijamii na yale ya kidini yanayoshughulikia tatizo hili yachunguze upya mikakati iliyopo na kutambua ile inayoweza kuboreshwa pamoja na mikakati mipya inayoweza kutekelezwa ili kukomesha tatizo hili hapa nchini.

Ushahidi ulioko umethibitisha kwamba wasichana wengi wasio na hatia bado wanakeketwa hapa nchini licha ya sheria, sera na miradi iliyoko ya kukomesha utamaduni huu. Ili kukomesha tatizo hili katika mwongo mmoja ujao wadau wanapaswa kutathmini juhudi za awali kwa lengo la kuboresha mikakati iliyowekwa. Hatima ya wasichana wengi hapa nchini inategemea utekelezaji mbinu mwafaka zitakazokomesha upashaji tohara wanawake. Lazima kuwe na juhudi za dharura kukomesha tatizo hili.

## Kumbukumbu

[1] Integrated Regional Information Networks (IRIN). *Africa: When Culture Harms the Girls-Globalization of Female Genital Mutilation* (Nairobi: IRIN, 2013).

[2] World Health Organization (WHO), *Eliminating Female Genital Mutilation: An Inter Agency Statement,* (Geneva: WHO, 2008).

[3] Kenya National Bureau of Statistics and ICF Macro, *Kenya Demographic and Health Survey 2008-09* (Calverton, Maryland: KNBS and ICF Macro, 2009).

[4] Isabel Mbugua, "Ending the Mutilation," *People and the Planet,* Vol. 6, No. 1, 1997.

[5] Heidi Jones et al., *Female Genital Cutting Practices in Burkina Faso and Mali and Their Negative Health Outcomes,* Stud Fam Plann 1999 Sep;30(3):219-30.

[6] WHO, "Female Genital Mutilation Programmes to Date – What works and what doesn't," *Policy Brief* WHO/RHR/11.36, <http://apps.who.int/iris/bitstream/10665/75195/1/WHO_RHR_11.36_eng.pdf>, accessed May 27, 2013.

[7] E. Banks et al., *Female Genital Mutilation and Obstetric Outcome – WHO collaborative prospective study in six Africa countries, Lancet* 2006 Jun 3;367(9525):1835-41.

[8] Kenyan Ministry of Health (MOH), *National Plan of Action for Elimination of Female Genital Mutilation.* Nairobi: MOH, 1999).

[9] National Coordinating Agency for Population and Development (NCAPD) *Sessional Paper No. 4 of 2000 on Population Policy for Sustainable Development* (Nairobi: NCAPD, 2000).

[10] Ministry of Gender, Sports and Youth, *Prohibition of Female Genital Mutilation Act* (Nairobi: Ministry of Gender, Sports and Youth, 2011).

[11] Law Society of Kenya, *The Kenya Constitution* (Nairobi: Law Society of Kenya, 2010).

[12] Charlotte Feldman-Jacobs and Donna Clifton, *Female Genital Mutilation/Cutting: Data and Trends Update 2010* (Washington, DC: Population Reference Bureau, 2010).

[13] KNBS and ICF Macro, Kenya Demographic and Health Survey 2008-09.

© 2013 Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD)